

## KAMATI NDOGO YA MAZINGIRA YAFANYA UKAGUZI KUONA HALI YA USAFI KATANI

Tarehe 10.10.2023, Kamati Ndogo ya Mazingira, ya Manispaa ya Morogoro ilifanya ziara kwenye Kata za Kingolwira, Boma na Mwembesongo kwa lengo la kuona jinsi uongozi wa Kata hizo unavyoshughulikia usafi wa mazingira kwa kuhakikisha taka zinakusanywa na kwenda kutupwa kwenye madampo yaliyowekwa na Manispaa.



Mwenyekiti wa Kamati hiyo, ambaye pia ni Diwani wa Kata ya Kihonda, Mheshimiwa Hamis Kilongo, akiwa katika ziara hiyo amewataka wananchi wafahamu kwamba suala la ulipaji wa ada ya taka sio hiari bali ni lazima na wote wanaogomea ama kukwamisha zoezi la ukusanyaji wa ada hiyo wachukuliwe hatua.



“Hakuna mtu ye yote anayekubaliana na suala la uchafu kwani kukubali uchafu ni kukubali maradhi, na ye yote anayekwamisha zoezi la ulipaji wa ada ya taka basi uongozi wa Kata hauna budi kumchukulia hatua stahiki” alieleza Mheshimiwa Kilongo.







Aidha, Kamati imependezwa na kupongeza uongozi wa Kata ya Boma kwa kufanikiwa kwa kiasi kikubwa kuweka mazingira ya Kata hiyo katika hali ya usafi na imetoa wito kwa uongozi wa Kata zingine kwenda kujifunza Boma namna ya kufanikisha zoezi la ukusanyaji wa taka na usafishaji wa mazingira katika Kata zao, huku huku ikiahidi kuhakikisha hali ya usafi wa mazingira ndani Manispaa ya Morogoro inaimarika zaidi kwa kuhakikisha uwepo wa mabwana na mabibi afya kwenye Kata zote za Manispaa.





**MWISHO**